

# MZOZO WA ASILI YA ULIMWENGU

Chris Sparks

# MZOZO WA ASILI YA ULIMWENGU

## Uchunguzi wa Kibiblia na Kihistoria wa Umbo la Dunia

Chris Sparks

EARTHEN VESSELS
2 CORINTHIANS 4:7

www.earthenvessels.org.au

# TUZINGATIE BIBLIA

Kwenye kipindi cha miaka mia tano iliyopita, nguvu za giza zimeendesha mashambulizi ya hatua kwa hatua dhidi ya sayansi ya kweli ya uumbaji wa Mungu. Ingawa Wakristo wengi wanaoiamini Biblia wanayashutumu mageuzi na nadharia inayoitwa Big Bang kwa ulaghai wa kishetani uliopo, kuna muunganiko mwingine kwenye mlolongo wa sayansi ya kughushi unaolidhihaki Neno la Mungu. Muunganiko huu unaonekana kwamba umeelekezwa kwenye rada, na si sehemu nyingine ila ni kwenye ulimwengu.

Wengi hudai kuwa, lugha inayotumiwa kwenye Biblia kuielezea Dunia ni ya mashairi kabisa; sio ya kisayansi. Inasemekana kuwa Biblia si kitabu cha kisayansi na hakipaswi kuwa hivyo. Ingawa kwa kweli Biblia ni yenye mashairi, kamwe usemi huo haukukusudiwa kuficha ukweli ulio wazi. Kinyume chake, lugha ya mashairi ilitumiwa kutoa uhai na uzuri kwenye ukweli. Ni mambo ya ajabu sana ya wanadamu ambayo yamefanya yale ambayo Mungu ameyaweka wazi kuwa ya ajabu. Mtume Paulo anatuonya juu ya mambo haya ya kipuuzi kwenye barua yake kwa Timotheo, akisema "elimu iitwayo elimu kwa uongo."

> 1 Timotheo 6:20 Ee Timotheo, ilinde hiyo amana; ujiepushe na maneno yasiyo ya dini, yasiyo na maana na mashindano ya elimu iitwayo elimu kwa uongo;

Ni nadharia zinazopinga sayansi ya kweli ya Biblia ambazo Paulo anazitaja kwa usahihi kuwa ni maarifa ya kughushi au kama "elimu iitwayo elimu kwa uwongo". Kwenye 2 Wakorintho 10:5, vile vile yeye anatusihi tutupilie mbali maarifa yote ya uongo ambayo yanajiweka yenyewe dhidi ya ujuzi unaopatikana kwenye Neno la Mungu:

> 2 Wakorintho 10:5 tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu;…

Kama mtu anakubali simulizi halisi ya uumbaji wa siku sita kwenye Kitabu cha Mwanzo sura ya 1, na kumheshimu Mungu siku ya saba aliyoitakasa, huu ni ushahidi wa imani. Hata hivyo, kama mtu atakataa ushuhuda

wa wazi wa kile ambacho Mungu alikiumba kwenye hizo siku sita, je, hii si kwa njia ile ile kuwa ni ishara ya kutoamini?

Leo sayansi kuu inakuza nadharia ya Big Bang na mageuzi/evolution kuwa kama ukweli. Pia, nadharia ya kuwa muundo wa kwamba Dunia ni tufe ambalo linazunguka kwenye mhimili wake na kulizunguka jua inakubaliwa kuwa ni ukweli usiopingika. Hata hivyo, hakuna imani yoyote kati ya hizi inayoweza kutegemewa kwenye Mwanzo 1, wala sehemu nyingine yoyote ya Neno la Mungu. Ni sababu hii inayomfanya Mwinjilisti JJ Davis aseme:

> Kwa ujumla, wainjilisti wamekuwa na msimamo kuwa masimulizi ya Mwanzo ya uumbaji yanahusika hasa kwenye maana na madhumuni ya kazi ya uumbaji ya Mungu na si maelezo kamili ya kisayansi…Tunatazamia sayansi ya chembe chembe za kijenetiki ili kujibu swali la kisayansi la lini ambapo maisha ya mwanadamu yanaanza na kwenye Biblia kupata majibu ya ufunuo kuhusu thamani na kusudi la maisha ya mwanadamu.[1]

Ni mawazo haya yaliyolegezwa ambayo yamewafanya watu wengi kutilia shaka mamlaka ya Neno la Mungu. Nadharia ya dunia yenye umbo la duara na kielelezo cha kuzunguka kwenye mhimili wake na kulizunguka jua imekubaliwa na wengi wanaodai kuiamini Biblia. Lakini baada ya uchunguzi, nadharia hizi hazipatani na Maandiko kabisa. Hatupaswi kushangaa kuwa wanadamu kama vile Daudi, Isaya, na Mfalme Sulemani wote waliamini kwenye kielelezo tofauti kabisa cha uumbaji. Watu hawa walipata ufahamu wao wa Dunia kutoka kwenye kitabu cha Mwanzo ambacho Musa aliandika kwa uthibitisho wa Mungu. Nukuu zifuatazo kutoka kwenye vyanzo vya ulimwengu, Kikristo, na Kiyahudi zinaonesha maoni ya sayansi ya asili ya dunia ambayo waandikaji wa Biblia wanaiamini:

> Waebrania wa mwanzo walifikiri kuwa ulimwengu ulifanywa na Dunia yenye umbo la diski ambayo ilikuwa ni kitovu cha ulimwengu, a0mbamo anga lililo kama kuba lilikuwa linashikiliwa na nguzo za mbinguni.
> - *National Centre for Science Education.*[2]
>
> Kwa kifupi, sayansi ya kale ya asili ya dunia ya Kiebrania, kama inavyo-

someka kwenye Agano la Kale inauzingatia ulimwengu ambao tunaishi kuwa ni diski tambarare, iliyofunikwa na kuba. Kitu kama stendi kubwa ya keki iliyofunikwa na moja ya kuba la glasi ya kawaida, ukipenda iwe hivyo.
- *Aletia Catholic Journal.*[3]

Waebrania waliichukulia Dunia kama tambarare au kilima chenye sura ya nusu tufe, inayoogelea juu ya maji. Juu ya hii ni kuba iliyowekwa imara kule mbinguni. Kwa kawaida imefungwa mwanga, nyota. Mwinuko huu ni mdogo sana kiasi kwamba ndege wanaweza kuinuka na kuruka kwenye anga lake.
- *Jewish Encyclopedia.*[4]




*WATERS ABOVE THE FIRMAMENT = MAJI JUU YA ANGA*
*Floodgates = Milango ya mafuriko*
*Stars = Nyota*
*Moon = Mwezi*
*Sun = Jua*
*Sheol = Kuzimu*
*Columns of the Earth = Nguzo za Dunia*
*OCEAN = BAHARI*
*Abyss = Shimo*
*Columns of Mountains - Nguzo za Milima*
*FIRMAMENT OF THE SKY = ANGA LA ANGA*
*EARTH = DUNIA*

Je, mtu afikiriwe kuwa mzushi kwa sababu anaitazama Dunia kwa mtazamo ulio sawa na waandikaji wa Biblia? Natumaini sio hivyo. Uhakiki rahisi wa Kitabu cha Mwanzo ungeufichua ulimwengu na kiwango kikubwa cha anga za juu kwenye sayansi ya uongo ambayo ipo. Inaposomwa kwa usahihi, mtu hupata mantiki rahisi kwenye simulizi aliyopewa Musa. Na tofauti na muundo wa kuwa dunia inazunguka kwenye mhimili wake na kulizunguka jua ambao unahitaji imani kwenye fizikia ya kinadharia, mtoto anaweza kuelewa kwa urahisi suala la Kitabu cha Mwanzo. Hebu sasa tukipitie Kitabu cha Mwanzo sura ya 1. Tukiruka nyuma ya uumbaji wa nuru siku ya kwanza, hebu turejee siku ya pili ya uumbaji:

> Mwanzo 1:6 Mungu akasema, Na liwe anga katikati ya maji, likayatenge maji na maji.
> 1:7 Mungu akalifanya anga, akayatenga yale maji yaliyo juu ya anga na yale maji yaliyo chini ya anga; ikawa hivyo.

Siku ya pili, shimo la maji liligawanywa kwenye miili miwili na muundo unaoitwa "anga". Anga lilitenganisha maji ya juu na maji ya chini, na kuunda anga katikati yake. Mtazamo sahihi wa anga ni ufunguo wa kuelewa kielelezo cha Biblia. Kwa Kiebrania, neno la 'anga' ni 'raqi ya`' (H7549). Neno hili linaonekana mara 17 tu kwenye Maandiko na lina maana maalum sana. Kinyume chake, neno 'mbingu' au (shâmayim) linaonekana mara 395, na lina maana pana zaidi.

Watu wengi hubishana kuwa neno 'raqiya` linamaanisha anga au utupu tu, kama inavyofafanua *Strong's Concordance*. Hata hivyo, hali hiyo haiwezi kuwa hivyo kwa kutegemea mambo mawili muhimu yaliyotajwa kwenye tukio la kwanza ambalo neno hilo linatokea.

Kwanza, kwenye Mwanzo 1:6-7 (siku ya pili ya uumbaji), tunaona kuwa anga ni kitu "kilichofanywa":

> Mwanzo 1:6 Mungu akasema, Na liwe anga katikati ya maji, likayatenge maji na maji.
> 1:7 Mungu akalifanya anga, akayatenga yale maji yaliyo juu ya anga na yale maji yaliyo chini ya anga; ikawa hivyo.

"Mungu *aliumba* anga". Hili linasemwa kinyume na kazi ambayo Mungu aliifanya siku ya kwanza ya uumbaji, Aliposema: “iwe nuru”. Tazama kutoka kwenye kifungu kifuatacho kuwa hakuna kitu kinachoonekana kilifanywa ili nuru ionekane siku ya kwanza.

> Mwanzo 1:3 Mungu akasema, Iwe nuru; ikawa nuru.
> Mwanzo 1:4 Mungu akaiona nuru, ya kuwa ni njema; Mungu akatenga nuru na giza.

Hakuna jengo la kimaumbile lililojengwa ili kuigawanya nuru na giza, kwa maana nuru na giza vyote ni vitu visivyoonekana kwa asili. Vile vile, utupu pia hauonekani na haushikiki. Kwa hivyo, kama anga si kitu zaidi ya utupu au uwazi, basi sio kitu ambacho kingehitaji kufanywa au kujengwa. Hata hivyo, hivyo ndivyo hasa inavyosemwa kuhusu anga kwenye Mwanzo 1:7.

Uthibitisho wa pili kuwa anga ni muundo thabiti ni kuwa kazi yake isiyopingika ni kushikilia sehemu kubwa ya maji. Ili kufanya hivyo, ni lazima lisipenyeze kitu na liwe ni lenye nguvu; sifa ambazo hakika hazipo kwenye sehemu iliyo tupu. Kwa hivyo, badala ya anga lenyewe kuwa ni sehemu tupu, uimara wa anga ni muhimu uwe na nafasi tupu. Hakika, mara tu muundo thabiti wa anga "ulipofanywa" ili kuyagawanya maji ya juu na maji ya chini, sehemu tupu au anga inaweza kuwepo katikati. Hii ndiyo sababu anga lilifanywa siku ya pili, kabla ya kuumbwa kwa nyota, mimea, na viumbe hai ambavyo siku zilizofuatia Mungu aliviweka chini yake. Kwa mfano, siku ya nne ya uumbaji, tunasoma hivi:

> Mwanzo 1:14 Mungu akasema, Na iwe mianga katika anga la mbingu ili itenge kati ya mchana na usiku; nayo iwe ndiyo dalili na majira na siku na miaka;
> 1:15 tena iwe ndiyo mianga katika anga la mbingu itie nuru juu ya nchi; ikawa hivyo.
> 1:16 Mungu akafanya mianga miwili mikubwa, ule mkubwa utawale mchana, na ule mdogo utawale usiku; akafanya na nyota pia.
> 1:17 Mungu akaiweka katika anga la mbingu, itie nuru juu ya nchi
> 1:18 na kuutawala mchana na usiku, na kutenga nuru na giza; Mungu akaona ya kuwa ni vyema.

Kwa njia sawa kama ambavyo mtu anavyoweza kuweka kiti au meza ndani ya nyumba, Mungu aliweka jua, mwezi, na nyota ndani ya anga. Hapo tunasema ndani ya anga iliyofanywa na muundo huo mgumu unaotenganisha maji. Kisha siku ya tano ya uumbaji, Mungu aliumba ndege wa angani na viumbe vya baharini. Kwenye mstari wa 20 tunasoma hivi:

> Mwanzo 1:20 Mungu akasema, Maji na yajawe kwa wingi na kitu kiendacho chenye uhai, na ndege waruke juu ya nchi katika anga la mbingu.

Ndege wa angani waliwekwa ndani ya anga lile lile lenye jua, mwezi, na nyota, kwa maana mstari huo unasema kuwa ndege hao "waruke juu ya nchi katika anga la mbingu." Wengine wanadai kuwa anga ambamo ndege huruka na anga ambamo viumbe vya mbinguni vipo ni sehemu mbili tofauti. Ila hii haiwezi kuwa hivyo, kwani neno lile lile la Kiebrania 'raqiya' linatumika kwenye sehemu zote mbili, na kwenye Mwanzo 1 hakuna palipotajwa kuwa kuna anga la ziada lililoundwa.

Kwa kuwa tafsiri sahihi ya anga ni muhimu kwenye kuielewa Biblia. mfano, tuchunguze maana yake kwa undani zaidi. Kama tulivyoona, neno la Kiebrania la anga ni 'raqiya'', ambalo linatokana na mzizi wa neno 'raqa''. Neno hili linatoa kidokezo cha jinsi maji yanavyoinuliwa juu ya anga:

> H7554 raqa`
> Mzizi wa asili; kupiga dunia (kama ishara ya shauku); kwa mlinganisho wa kupanua (kwa kupiga nyundo); kwa kudokeza kufunika (kwa karatasi nyembamba za chuma): - kupiga, kufanya kwa upana, kueneza nje (nje, juu, ndani ya sahani), mhuri, kunyoosha.[5]

Concordance inaielezea 'raqa`' kama hatua inayolinganishwa na usindikaji wa karatasi za chuma. Hii inaonyesha kwamba anga linaloshikilia maji juu lina nyenzo ngumu. Watafsiri wa Biblia walielewa hilo walipotumia neno 'imara' kwenye tafsiri yao ya neno hilo. Dhana hii ya kitu kigumu kinachobeba maji juu inapatikana kwenye Maandiko mengi na inaonekana iliaminiwa na waandishi wa kale. Kwa mfano, Elihu anastaajabia uhandisi wa Mungu kwa kuuliza swali lifuatalo kwa Ayubu:

> Ayubu 37:18 Je! Waweza kuzitandaza mbingu pamoja naye, Ambazo

zina nguvu kama kioo cha kuyeyushwa?

Hapa, neno la “kueneza nje” ni 'raqa`'; neno hilo hilo tumelichunguza hivi punde. Kwa akili ya Kiebrania, hii ingeleta taswira ya kuigonga nyenzo ngumu kama vile chuma. Neno hili pia limetumiwa na Musa kwenye Kitabu cha Kutoka katika kuuelezea uundaji wa dhahabu kuwa visahani vyembamba:

> Kutoka 39:3 Nao wakaifua hiyo dhahabu hata ikawa mabamba membamba sana, kisha wakaikata iwe nyuzi,...

Haitaleta maana endapo tutaitumia taswira kama hiyo kwenye kuelezea eneo tupu au anga. Wala mtu hatatumia maneno 'nguvu' au 'kuyeyushwa' (ambayo yanaashiria chuma cha kupondwa) kuelezea hewa. Badala yake, Elihu alielewa kuwa juu ya anga tunamoishi kulikuwa na mkanda thabiti wa kuakisi ambao unaweza kulinganishwa na kioo cha chuma. Kwenye akili ya Elihu, ni wazi kuwa mkanda huo ulihitaji kuwa na nguvu ili kubeba uzito mkubwa wa maji juu yake. Jambo la kufurahisha ni kuwa mchambuzi wa maoni ya Biblia, Albert Barnes alihitiimisha kwa kukubali vile vile, licha ya yeye mwenyewe kuamini kuwa Dunia ni tufe:

> ...dhana iliyoenea ilikuwa kwamba anga lilikuwa ni thabiti na lilikuwa ni mahali ambapo nyota zilishikiliwa...*Ambazo zina nguvu*—Imara, iliyoshikamana. Kwa uwazi ni kuwa Elihu alifikiri kuwa ilikuwa imara. Ilikuwa thabiti sana kiasi kwamba ilijitegemeza…*Na kama kioo cha kuyeyushwa*—Kama kioo kinachotengenezwa kwa kuunganishwa au kupondwa. Vioo vilitengenezwa kwa maganda ya chuma yaliyong'arishwa sana…*Hakuna shaka kuwa hofu ya mapema kuhusu anga ilikuwa, ni kwenye anga kuwa ni gumu*, na kwamba inasemwa hivyo mara nyingi kwenye Biblia.[6]

Kwa kumalizia, waandishi wa Biblia waliamini kuwa anga lina kitu kigumu. Hebu sasa tuchunguze baadhi ya vifungu vinavyoonesha jinsi walivyoliona umbo lake. Kutokana na vyanzo vya kihistoria vilivyotajwa hapo awali, *New American Standard Bible* inaelezea anga kuwa kwenye umbo la kuba:

Amosi 9:6 Yeye ndiye avijengaye vyumba vyake mbinguni, na kuweka misingi ya kuba yake juu ya nchi; yeye ndiye ayaitaye maji ya bahari, na kuyamwaga juu ya uso wa nchi; BWANA ndilo jina lake.

Ili anga liwe na umbo la kuba, ni lazima Dunia yenyewe iwe pande zote na tambarare. Kuba haliwezi kuwekwa juu ya tufe. Kwenye kitabu cha Isaya tunaona taswira ya anga ambalo ni sawa kulihusisha na umbo lake na ubora wake wa umbo:

Isaya 40:22 Yeye ndiye anayeketi juu ya duara ya dunia, na hao wanaokaa ndani yake huwa kama panzi; yeye ndiye azitandazaye mbingu kama pazia, na kuzikunja kama hema ya kukaliwa;

Ufahamu wa Isaya juu ya *umbo* la anga unaonekana kwenye maneno yake: "Azitandazaye mbingu kama pazia". Hili linaendana kikamilifu na dhana ya Elihu ya mbingu kuwa imara, kwani alisema hivi: "[Mungu] kuzitandaza mbingu pamoja naye, Ambazo zina nguvu kama kioo cha kuyeyushwa". Kudhania kuwa mistari hizi miwili (na mengineyo kama hiyo) hakuwakilishi chochote zaidi ya taswira ya mashairi ya kazi ya mikono ya Mungu, ni kuifanya kuwa haina maana. Ingawa hakuna anayeweza kukataa kuwa mistari hii imejaa tamathali za semi ambazo ni nzuri na hadhi ya mashairi, uzuri wake mkuu ni kulinganisha matendo kati ya mbingu (kipengele cha kazi ya mikono ya Mungu) na hema (kipengele cha kazi ya mikono ya mwanadamu). Kama vile hema linavyojipinda na kubadilika umbo juu ya sakafu tambarare na kuwalinda wakazi wake kutokana na hali ya juu yao, ndivyo ambavyo Bwana alivyoliinamisha anga imara juu ya Dunia ili kuwapa makazi viumbe Wake awapendao.





Lengo kuu la Isaya lilikuwa ni kukazia upendo wa Mungu wa kumpatia makazi mwanadamu. Bado huu ujumbe mzuri unaharibiwa pale mtu anapodai kuwa mistari ya Biblia haionyeshi chochote zaidi ya mashairi. Fikiria kifungu hiki kwa mara nyingine tena kwenye mtazamo wa ushahidi uliotolewa hivi punde:

> Isaya 40:21 Je! Hamkujua? Hamkusikia? Hamkuambiwa tokea mwanzo? Hamkufahamu tangu kuwekwa misingi ya dunia?
> 40:22 Yeye ndiye anayeketi juu ya duara ya dunia, na hao wanaokaa ndani yake huwa kama panzi; yeye ndiye azitandazaye mbingu kama pazia, na kuzikunja kama hema ya kukaliwa;

Kwenye huu muktadha, tunaona kuwa nabii anatoa karipio kali kwa wasikilizaji wake kabla ya kutoa maelezo yake ya Dunia kwenye mstari wa 22. Kimsingi, Isaya anaelekeza kwenye kanuni za uumbaji kuwa ni dhana za kimsingi ambazo wanaodai kuwa watu wa Mungu wanapaswa kuzijua na kuzielewa. Kwa nini? Isaya alikuwa tayari amewauliza watu kwenye mstari wa 18: “Basi, mtamlinganisha Mungu na nani? Au mtamfananisha na mfano wa namna gani?” Mambo ya hakika ya uumbaji yanamshuhudia Mungu mtukufu, mwenye upendo, na anayejali, kama kielelezo cha hema kinavyoonesha kikamilifu.

Kumbuka kuwa kwenye hii sura, Isaya anazungumza na watu wa Israeli wanaoabudu sanamu. Na ni tofauti kabisa na miungu yao ya uongo—ambayo ilikuwa ni “kazi ya mikono ya wanadamu, miti na mawe, isiyoona, wala kusikia, wala kula, wala kunusa”—ndipo Isaya anaangazia ukuu na uzuri wa Mungu juu ya uumbaji. (Tazama Kumbukumbu la Torati 4:28) Kwa kweli, Isaya atumia mambo ya uhakika ya uumbaji kuwa ndiyo uthibitisho wa kuwa Mungu mmoja wa kweli ana madaraka ya utendaji wa kuvitunza viumbe Vyake.

Kuhusiana na neno ‘mzunguko’ kwenye Isaya 40:22, ina maana ya kile tu inachokisema. Isaya alijua neno la kuhusu tufe kwa sababu kwenye Isaya 22:18, anasema kuwa Mungu angewarusha watu Wake waasi “kama mpira” (akitumia neno la Kiebrania 'dûr'). Hata hivyo, anaporejelea Dunia kwenye sura ya 40, Isaya anatumia neno la Kiebrania 'chûg' (ambalo linamaanisha duara) kuonesha kwamba ni duara lakini ni bapa.

Kwenye hili suala, mtu anaweza kujiuliza ni nini kinachoizuia bahari kutoka kwenye kingo za Dunia ambayo ni tambarare. Jibu linapatikana kwenye Mithali 8, ambapo Yesu anashuhudia kuwa alikuwepo wakati Mungu "Alipoipa bahari mpaka wake, kwamba maji yake yasiasi amri yake; alipoiagiza misingi ya nchi;" Mithali 8:29. Hilo linathibitishwa na Ayubu anayesema hivi: "Amepiga duara kuwa ni mpaka juu ya uso wa maji, Hata hapo mwanga na giza vinapopakana." Ayubu 26:10. Inashangaza, mstari huu haufundishi tu kuwa Mungu ameweka mpaka wa maji, lakini kuwa mpaka huu upo kwenye umbo la duara. Kwa hakika, neno la Kiebrania la "kuzungukwa" ni neno 'chûg', ambalo concordance inafafanua kama: "kuelezea duara". Kwa hiyo, kama vile ambavyo mtu angetumia dira katika kuchora duara, mstari huu unaonesha kuwa Mungu ameweka mpaka wa mviringo kwa ajili ya maji. Kwenye Zaburi 104, Daudi anarejelea mipaka inayoyazunguka maji. Anasema hivi: "Umeweka mpaka yasiupite, Wala yasirudi kuifunikiza nchi." Zaburi 104:9.

Zaidi ya hayo, kwenye maelezo yake juu ya Isaya 40:22, Albert Barnes anasema hivi: "Wakati huo umbo la tufe lote halikujulikana; na wazo lililopo ni kuwa, Mungu aliketi juu ya mzunguko huu ulioongezwa, au duara; na kuwa dunia kubwa ilikuwa chini ya miguu yake." Kama ilivyotajwa mapema, Albert Barnes mwenyewe aliamini kuwa kuna ulimwengu, lakini anakubali kuwa Waebrania hawakuamini, kwa kuwa wakati huo wazo la Dunia yenye duara halikujulikana kabisa. Badala yake, Barnes anatafsiri Isaya 40:22 kwa uhalisia, kama vile Waebrania walivyofanya, na wala hahusishi neno 'duara' kuwa tafsiri ya mashairi ya neno 'duara'. Barnes anasema kuwa kwa mtazamo wa Isaya, Mungu anakaa juu ya duara tambarare la Dunia. Hata hivyo Isaya hakuwa pekee yake kwenye kuyashikilia haya maoni. Nabii Ezekieli alikuwa na bahati wa kuliona anga, ambapo anasema hivi: "mbingu zilifunuka, nikaona maono ya Mungu". Ezekieli 1:1. Ufafanuzi wa Ezekieli juu ya anga ni kama ifuatavyo:

> Ezekieli 1:22 Tena juu ya vichwa vya viumbe hai palikuwa na kila mfano wa anga, kama rangi ya bilauri, lenye kutisha, limetandwa juu ya vichwa vyao.

Kulingana na Ezekieli, anga hilo limetengenezwa kwa kitu kigumu, kinacholingana na kioo. Sasa angalia kile ambacho Ezekieli alikiona upande

wa pili wa anga:

> Ezekieli 1:26 Na juu ya anga, lililokuwa juu ya vichwa vyao, palikuwa na mfano wa kiti cha enzi, kuonekana kwake kama yakuti samawi; na juu ya mfano huo wa kiti cha enzi ulikuwako mfano kama kuonekana kwa mfano wa mwanadamu juu yake.

Ezekieli aliona kuwa kiti cha enzi cha Mungu kilikuwa juu ya anga lililoifunika dunia. Hili linapatana kikamilifu na ushuhuda ufuatao kutoka kwa Musa:

> Kutoka 24:10 wakamwona Mungu wa Israeli; chini ya miguu yake palikuwa na kama sakafu iliyofanyizwa kwa yakuti sawami, kama zile mbingu zenyewe kwa usafi wake.

Pia, Musa alimwona Mungu wa Israeli akiwa ameketi kwenye kiti chake cha enzi huko mbinguni, na akabainisha kuwa chini ya miguu yake kulikuwa na kitu kigumu ambacho kilionekana kama "*sakafu* iliyofanyizwa kwa yakuti sawami". Jambo la kushangaza ni kuwa neno la Kiebrania la 'sakafu' ni neno 'libnâh' (H3840), ambalo linatokana na mzizi wa neno 'lâban' (H3835). Neno hili linamaanisha "weupe, yaani, (kwa maana) uwazi".[7] Kwa kuzingatia hili, *Young's Literal Translation* ya Kutoka 24:10 inasomeka hivi:

> Kutoka 24:10 wakamwona Mungu wa Israeli; chini ya miguu yake palikuwa na *kama sakafu iliyofanyizwa kwa yakuti sawami*, kama zile mbingu zenyewe kwa usafi wake.

Musa aliona kuwa chini ya miguu ya Mungu kulikuwa na sakafu ambayo ilikuwa na muonekano wa "sakafu iliyofanyizwa kwa yakuti sawami". Ingawa kwa ujumla yakuti samawi hufikiriwa kuwa na rangi ya samawati, kwa kweli kuna yakuti nyeupe. Inajulikana kuwa yakuti samawi hupokea rangi "kutokana na vitu vilivyomo duniani wakati madini ya kung'ara yanafanyizwa." Ni hivyo ikawa "yakuti nyeupe ni adimu kabisa; hazijaguswa kabisa na vipengele vya kufuatilia."[8]

Musa anaelezea kwa uwazi juu ya lile lile anga lililonenwa na Ezekieli. Kwa

maana kwenye mstari wa 22, Ezekieli anafafanua kuwa anga ni "kama rangi ya *bilauri*, lenye kutisha, limetandwa juu ya vichwa vyao." Yakuti nyeupe ni madini ya kung'ara yasiyo na rangi kabisa. Ni wazi, ndiyo maana neno la Kiebrania 'libnâh' limetumiwa, na kwa nini Musa anasema kuwa chini ya kiti cha enzi cha Mungu palikuwa na "kama sakafu iliyofanyizwa kwa *yakuti sawami*, kama zile mbingu zenyewe kwa *usafi* wake." Madini ya kung'ara ya yakuti huleta ubora wa kushangaza kweli. Mizani ya Moh—ambayo huuorodhesha ugumu wa madini ya mchimbaji kutoka kwenye kipimo cha 1–10—huyaweka yakuti (muundo wa madini ya kung'ara) kwenye kipimo cha 9. Ni ajabu, almasi ndiyo madini pekee ambayo ni magumu zaidi kuliko yakuti, yakiwa na orodha ya 10 kwenye mizani ya Moh.[9]

Kwa kulizingatia hilo, anga—kama lilivyoonwa kwenye maono ya Ezekieli na Musa—linafananishwa na muundo ulio wazi lakini ambao ni thabiti sana. Zaidi ya hayo, wanaume hawa wote wawili waliona kuwa kiti cha enzi cha Mungu kilikuwa juu ya muundo huu. Na bado, tulijifunza mapema kuwa kuna maji juu ya anga, kwa kuwa kusudi lake ni kuyatenganisha maji ya juu na maji ya chini. Basi ni kwa jinsi gani kiti cha enzi cha Mungu kipo juu ya anga, wakati nafasi hiyo inakaliwa na maji? Fikiria kifungu kifuatacho kutoka kwenye Zaburi 104, ambamo mtunga zaburi anaubainisha uzuri wa maelezo ya Ezekieli ya kiti cha enzi cha Mungu juu ya anga, pamoja na maarifa ya maji yaliyoinuliwa juu:

> Zaburi 104:3 Na kuziweka nguzo za orofa zake majini, huyafanya mawingu kuwa gari lake, Na kwenda juu ya mabawa ya upepo,

Mungu ameiweka mihimili ya vyumba vyake ndani ya maji juu ya anga. Kwa mara nyingine tena, Albert Barnes anafafanua hitimisho lile lile:

> Neno "maji" hapa linarejelea maelezo ya uumbaji kwenye Mwanzo 1:6-7 – maji ya "juu ya anga," na maji ya "chini ya anga." Dokezo la hapa ni maji yaliyo juu ya anga; na maana yake ni kuwa, Mungu alikuwa amejenga mahali pa makao yake mwenyewe - chumba alichokuwa akikaa kwenye hayo maji; yaani, mahali palipotukuka zaidi kwenye ulimwengu. Haimaanishi kuwa alitengeneza kwa maji, bali—makao yake—yalikuwa ndani au juu ya maji hayo, kana kwamba hakujenga makao yake

juu ya udongo au mwamba, bali ndani ya maji, akiweka uthabiti pale ambapo hapakuwa na uthabiti, na kuyafanya maji yenyewe kuwa msingi wa muundo wa makazi yake.




*HEAVENS OF THE HEAVENS = MBINGU ZA MBINGU*
*Waters above the Firmament = Maji yaliyo juu ya anga*
*Divine Dwelling = Makao ya Mungu*
*Firmament = Anga*
*HEAVENS = MBINGU*
*Sun = Jua*
*Moon = Mwezi*
*Stars = Nyota*
*Earth = Ardhi*
*Sea = Bahari*
*UNDERWORLD = ULIMWENGU*
*Foundations of the Heavens = Misingi ya Mbingu*
*Waters below the Firmament = Maji chini ya anga*
*Foundations of the Earth = Misingi ya Dunia*

Kwa mara nyingine tena, kanuni hii inaangazia upendo na wema wa Mungu juu ya uumbaji. Badala ya kujiweka mbali na mabilioni ya miaka ya nuru, Mungu wetu ana kiti Chake cha enzi juu tu ya anga, na daima anatazama na kuwatunza wakaaji wa Duniani, waliopo chini! Bado hakuna hata moja kati ya aya hizi yenye umuhimu wowote kwenye modeli ya kwamba dunia inazunguka jua na kuzunguka kwenye mhimili wake. Kwa maana kwenye mfumo wa jua, inadaiwa kuwa "hakuna anga, na hakuna maji juu yake."[10] Vitabu vya kiada vya sayansi vipo kimya kabisa juu ya uwepo wa anga na maji juu kwa sababu rahisi ambayo sayansi inashutumu uwepo wao. Na bado huu ndiyo mfano ambao Wakristo wengi wanachagua kudumisha na kuutetea.

## Dunia Ina Misingi

Tamko lingine la Maandiko linalorudiwa mara kwa mara ni kuwa Dunia imejengwa juu ya misingi. Nabii Samweli anafafanua misingi hiyo kuwa ni nguzo: "Kwa maana nguzo za dunia zina BWANA, Naye ameuweka ulimwengu juu yake." 1 Samweli 2:8. Zekaria anathibitisha jambo hilo hilo: "Ufunuo wa neno la BWANA juu ya Israeli. Haya ndiyo asemayo BWANA, azitandaye mbingu, auwekaye msingi wa dunia". Zekaria 12:1. Mtu anaweza kusema kuwa mistari hii ni ya mashairi tu; kuwa Dunia haijajengwa juu ya nguzo halisi. Bado dhana hii inawasilishwa na Muumba Mwenyewe. Mungu anazungumza na Ayubu kwa sauti na kusema: "Ulikuwa wapi nilipoiweka misingi ya nchi? Haya! Sema, kama ukiwa na ufahamu." Ayubu 38:4. Kwenye mstari wa 6, Mungu anarudia suala Lake kwa kuuliza: "Misingi yake ilikazwa juu ya kitu gani?"

Je, Mungu angemjibu Ayubu swali ambalo lilikuwa ni la mafumbo? Je, Mungu angempa changamoto Ayubu kwa swali ambalo halingeweza kujibiwa kwa sababu hakuna misingi ya kweli? Hiyo haitakuwa changamoto ya haki au uaminifu. Ukweli ni kuwa Mungu mwenyewe anazungumza na Ayubu na mara mbili anasema kuwa ameweka misingi ya Dunia. Na bado, Mkristo anayeamini kwenye ulimwengu unaozunguka angani hawezi kukubali maneno haya kuwa ni maneno halisi, ingawa yalisemwa na Mungu Mwenyewe kuhusu uumbaji Wake mwenyewe. Huu ni mfano mkuu wa jinsi dhana ya dunia kuzunguka kwenye mhimili wake na

kulizunguka jua inawaongoza watu kulitilia shaka Neno la Mungu.

Dunia ina misingi, na kama tulivyoona tangu siku ya kwanza ya uumbaji, misingi hii iliwekwa juu ya maji ya kilindi kikuu. Kwa mara nyingine tena *The Jewish Encyclopedia* inathibitisha kuwa hivi ndivyo Waebrania walivyoamini:

> …Waebrania waliamini kuwa hapo mwanzo, kabla ya dunia na mbingu kutenganishwa, kulikuwa na bahari kuu na giza. Kutokana na hili "neno la Mungu" lilitoa nuru. Aliyagawanya maji: Maji ya juu aliyaweka mbinguni, Na chini yake aliiweka dunia.[11]

Ufahamu huu wa siku ya kwanza ya uumbaji unapatana kikamilifu na vifungu vingine vingi vya Maandiko. Kama vile mtungaji wa zaburi asemavyo: "Maana ameiweka misingi yake juu ya bahari, Na juu ya mito ya maji aliithibitisha." Zaburi 24:2. Wakati wa gharika hiyo, "chemchemi zote za vilindi vikuu zilibubujika kwa nguvu, madirisha ya mbinguni yakafunguka." Mwanzo 7:11. Maji yaliyoijaza dunia yalitoka juu na chini. Lakini madirisha ya anga yalipofunguliwa, siyo maji yote ambayo hayakulegezwa. Kwenye Mwanzo 8:2 tunaona kuwa baada ya muda fulani, Mungu aliyafunga madirisha ya mbinguni na maji yakazuiliwa. Mstari huo unasema hivi: "chemchemi zote za vilindi vikuu zilibubujika kwa nguvu, madirisha ya mbinguni yakafunguka" Zaidi ya hayo, Daudi alisema hivi muda mrefu baada ya gharika: "Msifuni, enyi mbingu za mbingu, nanyi maji mlioko juu ya mbingu." Zaburi 148:4. Anga na maji yaliyo juu yapo hadi leo!

## Dunia Imetulia na Jua Linasogea

Mungu aliagiza kuwa itakuwa ni kazi ya jua na mwezi kuamuru siku, usiku, majira na miaka ambayo wanadamu wangepitia hapa Duniani. Kinyume chake, muundo wa dunia kuzunguka kwenye mhimili wake na kulizunguka jua unathibitisha kuwa ni jukumu la Dunia kutengeneza siku, misimu, na miaka kwa kuzunguka kwenye mhimili wake na kulizunguka jua. Hilo linawekwa mbali na muhtasari wa Mwanzo 1:14, ambapo Mungu anasema kuwa jua na mwezi zilitakiwa "itenge kati ya mchana na usiku; nayo iwe ndiyo dalili na majira na siku na miaka.

Zaidi ya hayo, ni muhimu kutambua kuwa Dunia imelitangulia jua. Kama tulivyoona, jua liliumbwa siku ya nne na liliwekwa ndani ya anga lililoundwa na anga juu ya Dunia. Kulingana na simulizi hili, Dunia inawezaje kulizunguka jua? Rudi kwenye kielelezo kilichooneshwa hapo awali na utaona kuwa haiwezekani kwa Dunia—ambayo ni msingi—kulizunguka jua ambalo limezuiliwa kwenye nafasi iliyo juu yake. Huu ni mfano mmoja wa jinsi muundo wa dunia kulizunguka jua na kuzunguka kwenye mhimili wake hauendani kabisa na suala la Mwanzo.

Zaidi ya hayo, kwenye Zaburi 93:1, tunaambiwa kuwa "ulimwengu umethibitika usitikisike." Hili limerudiwa karibu neno kwa neno kwenye 1 Mambo ya Nyakati 16:30: "naam, ulimwengu umethibitika usitikisike;" Kinyume chake, tunaambiwa kwenye vifungu vingi kuwa jua linasogea. Kwenye Zaburi 19:1, Daudi anasema hivi: "Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu, Na anga laitangaza kazi ya mikono yake." Anga ni mada ambayo inapaswa kuchunguzwa kwa sababu inaangazia ukuu wa Mungu aliye bora na mkamilifu. Hili ndilo jambo ambalo Isaya analieleza kwenye sura ya 40 ya kitabu chake. Daudi anaendelea kusema:

> Zaburi 19:4 Katika hizo [mbingu] ameliwekea jua hema,
> 19:5 kama bwana arusi akitoka chumbani mwake, Lafurahi kama mtu aliye hodari Kwenda mbio katika njia yake.
> 19:6 Kutoka kwake lautoka mwisho wa mbingu, Na kuzunguka kwake hata miisho yake, Wala kwa hali yake Hakuna kitu kilichositirika.

Mtu anawezaje kuoanisha kifungu hiki—ambapo Daudi analilinganisha jua na mwanaume mwenye nguvu anayekimbia kwenye mbio na bwana arusi anayetoka kwenye chumba chake—na kielelezo cha kitovu cha anga? Je, mtu anawezaje kuyaoanisha madai ya Daudi kuwa jua hutembea kwenye mzunguko, kwa imani kuwa ni Dunia ambayo huzunguka na kulizunguka jua? Kwa mara nyingine tena, tunaona kuwa Biblia na mtazamo wa dunia kulizunguka jua na kuzunguka mhimili wake hauendani kabisa.

Kama mtu anasimamia kwenye Maandiko, lazima wahitimishe kuwa ni jua linalotembea; sio Dunia. Hata hivyo, kama Ayubu anavyokiri, Mungu ana uwezo wa kulifanya jua lisimame, kama ilivyokuwa mbele ya Yoshua

wakati "jua likasimama kimya katikati ya mbingu." Yoshua 10:13. Ayubu anasema kuwa Mungu "Aliamuruye jua, nalo halichomozi;" Ayubu 9:7. Kwa wale wanaokubali kielelezo cha Biblia, si vigumu kuwazia jua limesimama tuli katikati ya anga lililoundwa na anga. Vile vile haitumiki kwa wale wanaoshikilia mfano wa dunia kuzunguka kwenye mhimili wake na kulizunguka jua. Mtindo huu haufikirii tu kuwa Dunia inazunguka kwenye mhimili wake na kuzunguka jua, lakini kuwa mfumo mzima wa jua unajichaji kupitia anga kwa kasi ya kilometa 828,000 kwa saa. Yoshua anabainisha kuwa Mungu aliamuru jua lisimame na 'halikufanya haraka kutua kama siku nzima. Kama Dunia ingewekwa tuli kwa masaa 12, ingekuwa karibu kilomita milioni 10 nyuma ya mfumo wa jua. Je, haileti maana zaidi kumkubali Mungu kwenye Neno Lake, na kukubali kuwa jua ndilo lililosimama tuli katikati ya mbingu, kama vile Yeye asemavyo?

Mtu anapolizingatia Neno la Mungu kwa njia hii, matokeo yake ni ya ajabu sana. Tunaona kuwa hatulizunguki jua; dhana ambayo ina mizizi yake kwenye ibada ya kipagani na ibada ya jua. Zaidi ya hayo, hatuungwi mkono na kile kinachoitwa mvuto wa jua. Kwani Mungu anakuwa anafanya "kuutundika ulimwengu pasipo kitu". Ayubu 26:7. Mungu ndiye anayeishikilia Dunia ikae mahali pake. "Nimezisimamisha nguzo zake," Anasema kwenye Zaburi 75:3. Hakika, Dunia ni kitovu cha mpango wa Mungu. Tunaimarishwa na nguvu zake, na kweli ni mboni ya jicho Lake.

Kwa ajili hiyo, tumeona kuwa waandishi wa Biblia waliamini kwenye kielelezo cha Dunia kuwa ni tambarare, wakiutegemeza ufahamu wao juu ya Mwanzo na Maandiko ya Agano la Kale. Kwenye hii modeli, uso wa Dunia umesimama ili kuwa na uso tambarare, wa duara ambao juu ulipasuliwa na muundo unaofanana na hema unaoitwa anga. Anga ni lenye muundo thabiti ambao huyashikilia maji juu na kudumisha mgawanyiko wao kutoka kwenye maji yaliyo chini. Na jua, mwezi, nyota na ndege wa angani hukaa kwenye anga lililoumbwa na anga.

Kwenye sehemu inayofuata ya kitabu hiki, tutachunguza historia ya asili ya ulimwengu, tukifuatilia kutoka kwenye namna tunavyoyaelewa maandiko ya Kiebrania hadi kwenye maoni yanayokubalika sana hii leo. Tutafichua jinsi ilivyo, lini, na nani aliyeanzisha nadharia ya ulimwengu, na tutaichunguza mihimili ambayo nadharia hii mpya imekuwa nayo wakati huo na mpaka sasa.

# HISTORIA YA ASILI YA ULIMWENGU

Ni jambo lisilo na shaka kuwa Waebrania wa kale walifikiri kuwa Dunia ipo tambarare, isiyozunguka. Hili limethibitishwa si tu kwa upatano wa wanahistoria wa ulimwengu na wanathiologia ya mambo ya kidini, bali kutoka kwenye Biblia yenyewe. Hebu sasa tuichunguze asili ya mfano wa dunia kulizunguka jua na kujizungusha kwenye mhimili wake na ulimwengu unaozunguka. Haishangazi, dhana hii imeanzishwa kwenye falsafa ya kipagani, kama yalivyo mafundisho mengi yasiyofuata maandiko. *Encyclopaedia Britannica* inasema hivi:

> Kwa kawaida, kukubali wazo kuwa Dunia ni duara hutolewa kwenye Pythagoras (iliyostawi kwenye karne ya 6 KK) na mafundisho yake…[12]

Inapendeza, Origen na Augustine—mababa wa kanisa ambao makosa mengi ya Ukristo yanaweza kuhusishwa nao—waliathiriwa sana na mawazo ya Plato. Kuhusu Dunia, Pythagoras na Plato walifundisha *dunia kuwa ni duara*. Muundo wa kwanza wa *dunia kulizunguka jua na kuzunguka kwenye mhimili* wake unawekwa kwa Aristarchus, kama nukuu ifuatayo inavyosema:

> Mwanaastronomia Mgiriki wa karne ya 3 KK, Aristarchus of Samos alikuwa ni mwanzilishi wa nadharia ya kuwa Jua lipo katikati ya ulimwengu na kuwa Dunia inalizunguka.[13]

Kanisa la kwanza la Kikristo halijasemekana kwamba lilizipitisha dhana hizi za kipagani. Na wakati wa enzi za giza, nadharia ya dunia kuzunguka kwenye mhimili wake na kulizunguka jua (pamoja na masomo yote) ilijikita katikati ya giza la Kirumi. Hata hivyo, kwa sababu ya kuongezeka tena kwa haraka kwa ujuzi wa Biblia mapema kwenye karne ya 16, shambulio jipya lilifanywa na nguvu za giza dhidi ya ukweli wa Neno la Mungu. Ili imani kwenye Maandiko iweze kuondolewa tena kutoka kwenye mioyo ya watu, ufunuo wa Mungu uliwekwa kwenye mafundisho ya wanafalsafa.

Nukuu ifuatayo imeandikwa na Andrew Dickson White; mwanamageuzi na msaidizi wa mfano wa dunia kulizunguka jua na kuzunguka kwenye mhimili wake. Akiwa hana upendeleo wowote kwenye kielelezo cha Biblia, White anafichua ushindi uliopatikana juu ya simulizi ya Mwanzo wa uumbaji kupitia nadharia za watu watano:

> Kwenye nusu ya mwisho ya karne ya kumi na sita hawa wanamageuzi wa nadharia [nadharia zinazoelezea uumbaji halisi wa siku 6] ulionekana kuwa na umbo dhahiri zaidi…Kwa maana walikuja, mmoja baada ya mwingine, watano kati ya watu wakuu zaidi wa jamii ulimwengu iliwazalisha—Copernicus, Kepler, Galileo, Descartes, na Newton—*na wakati kazi yao ya dhana ya zamani ya kitheolojia ya ulimwengu ilipomalizika, ukweli kuhusu uumbaji ilipotea*. "Anga pana lililo juu "—"nyuzi za uangavu"—Mweza wa Yote aliketi juu ya "duara la mbingu," na kwa mikono yake mwenyewe, au pamoja na malaika wakiwa wawakilishi wake, akiliweka jua, mwezi, na sayari kwa ajili ya ulimwengu. Faida ya dunia, kufungua na kufunga "madirisha ya mbinguni," akishusha juu ya dunia "maji yaliyo juu ya anga," "akiweka upinde wake mawinguni," yaking'inia kwenye "ishara na maajabu," kurusha nyota, "kuweka radi" ili kuwatisha waovu, na "kuitikisa dunia" kwenye ghadhabu yake: *haya yote yalikuwa yametoweka*. Watu hawa watano walikuwa wametoa ufunuo mpya wa kiungu kwenye ulimwengu; na kupitia yule wa mwisho, Newton, alikuja na dhana mpya ambayo ni kubwa, *iliyokusudiwa kuwa mbaya kwenye nadharia ya zamani ya uumbaji…watu hawa walitoa msingi mpya wa nadharia ya mageuzi inayotofautishwa na nadharia ya uumbaji*.[14]

Kwa kushangaza, kiini cha kifungu hiki kipo wazi. Kazi ya Copernicus, Kepler, Galileo, Descartes, na Newton ilikuwa mbaya kwenye nadharia ya uumbaji. Kazi yao ilifungua njia kwenye nadharia ya mageuzi na baadaye ikaja nadharia ya Big Bang. Sasa, kwa kifupi, tuichunguze kazi ya baadhi ya watu hao.

## Copernicus: Aliidhinishwa na Roma

Nicolaus Copernicus anatajwa kuwa ndiye aliyekuwa chanzo cha kuleta nadharia ya dunia kuzunguka mhimili wake na kulizunguka jua kwa

Wakristo wa Magharibi. Kabla ya mawazo ya Copernicus kuenea, kwa kawaida ilikuwa ni kwamba Dunia—wala si jua—ilikuwa ndiyo kitovu cha anga.

Copernicus aliishi wakati wa kilele cha matengenezo ya kanisa. Aliishi wakati wa Martin Luther, John Calvin, William Tyndale, na Huldrych Zwingli, pamoja na wanaharakati wengine wengi wa Kiprotestanti. Hata hivyo, tofauti na watu hao wenye ujasiri, Copernicus hakukubali mawazo ya kimapinduzi ambayo yalikuja na ufufuo wa ujuzi wa Biblia. Kwa kurejelea kitabu cha Angus Armitage *Copernicus, the Founder of Modern Astronomy* (1990), Robert J. Spitzer anatoa maoni yafuatayo:

> Copernicus alikuwa ni Mkatoliki muaminifu ambaye aliyachukua maagizo madogo kama kasisi wa Kikatoliki na alikuwa wakili wa kanuni za ndani ya Kanisa Katoliki.[15]

Uchambuzi wa wakati ambapo matokeo ya Copernicus yalichapishwa unaonyesha wazi mbinu za adui kupotosha kweli. Kuongoza hadi wakati ambapo kitabu cha Copernicus kilipochapishwa, Upapa ulikuwa umepoteza mshikamano wao kwenye akili za wanadamu. Chombo cha kugundua makosa ambayo ni—Maandiko Matakatifu—hatimaye iliwekwa karibu na watu wa kawaida. Na kwa uvumbuzi wa Johannes Gutenberg wa mashine ya kuchapisha inayoweza kuhamishika mnamo mwaka 1450, Biblia ilikuwa inapatikana kwa bei nafuu. Mnamo mwaka 1516, Erasmus alitoa hati ya Kigiriki iliyotakaswa, inayojulikana kama *Textus Receptus*, ambayo ndiyo ikawa ni msingi wa tafsiri ya Martin Luther ya Agano Jipya kwenye lugha ya Kijerumani mwaka 1522, na baadaye tafsiri ya Kiingereza ya William Tyndale mwaka 1534. Kama mwanahistoria, Benjamin Wilkinson anavyoandika kuwa:

> Upapa wa zama za kati uliamka kutoka kwenye ulegevu wake wa kishirikina kuona kuwa kwenye theluthi moja ya karne, Matengenezo ya Kanisa yalikuwa yamechukua theluthi mbili ya Ulaya. Ujerumani, Uingereza, nchi za Skandinavia, Uholanzi, na Uswisi zilikuwa ni za Kiprotestanti. Ufaransa, Poland, Bavaria, Austria, na Ubelgiji pia zilikuwa zikiyumba kwa njia hiyo.[16]

Mnamo mwaka 1517, Martin Luther alipigilia misumari zaidi ya mashtaka 95 kwenye mlango wa Kanisa la Castle huko Wittenberg, na kuashiria mwanzo wa ukombozi wa Kiprotestanti. Miaka ishirini na sita baadaye, maelezo ya Copernicus kuhusu dunia kuzunguka jua na kuzunguka kwenye mhimili wake yalichapishwa kwenye kitabu chake, *On the Revolutions of the Heavenly Spheres*, kilichotolewa mwaka 1543. Kufikia hatua hii, kuwepo kwa upapa ulikuwa unatishiwa kupitia kusambazwa sana kwa Bibilia. Kwa hiyo, inaweza kuwa si kwa bahati kwamba wakati huu ndipo kitabu cha Copernicus kilipochapishwa. Na kama ilivyoelezwa hapo awali, mwana astronomia huyo mwenye mvutano mkubwa alikuwa ameingiza nadharia ya dunia kuzunguka jua na kuzunguka kwenye mhimili wake kutoka kwenye maandishi ya wanafalsafa ambao ni wapagani.

Akidumisha upatano ambao ni kamili na simulizi ya Mwanzo, hapa Daudi anasema kuwa Dunia imewekwa juu ya maji ya kilindi kikuu; kuwa thabiti juu ya yale ambayo hayana uthabiti. Wazo linalowasilishwa na Ayubu na Daudi ni kuwa ni uweza wa Mungu unaoipa Dunia uthabi-

ti. Zaidi ya hayo, mtume Paulo anasema kwenye Waebrania 1:3 kuwa ni Mwana wa Mungu ambaye huwa "akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake," Bado sayansi ya kisasa inatafuta kuhusisha nguvu hii na chembe za phantom.

Kwa dhana hizi za miungu, je, unaanza kuona hila inayofanywa kuelekea maslahi ya Muumba wetu kwenye ulimwengu wetu? Bila shaka, ile inayoitwa sheria ya asili ya mvutano imechukua sehemu ya utendaji wa daima na wa kimuujiza wa Mungu, ambao manabii wa kale waliustaajabia.

Kwa hiyo, setilaiti zilizo kwenye obiti, usafiri wa angani na kitu kingine chochote ambacho kinategemea nadharia ya Newton ya nguvu ya mvutano inaweza kuzingatiwa kuwa ni ya uongo, bila kujali jinsi ustadi wa SpaceX au NASA na picha zao zinazozalishwa na kompyuta zinavyoweza kuonekana. Kiasi kidogo cha utafutaji upya kitayafichua wazi wazi haya mashirika na safari yao ya anga la juu inayodhaniwa kuwa ni ulaghai wa kina. Na mtafutaji ukweli ambaye ana bidii atajua kuwa kuna majibu ya kutosha kwenye maswali ambayo yanaweza kutokea kuhusu mawasiliano ya simu na teknolojia nyinginezo za teknolojia.

Historia ya dunia kulizunguka jua, na sifa za kutiliwa shaka za vyombo vilivyoipeleka kwenye ulimwengu wa Kikristo, inapaswa kuwa sababu ya wasiwasi mkubwa kwa Mkristo yeyote anayeamini kwenye ulimwengu. Kazi ya watu hawa, pamoja na mawazo yao yanayochangamana na hesabu za kuchekesha, imesababisha Neno la Mungu pamoja na asili rahisi ya ulimwengu ionekane kutokuwa na akili. Kadri tufe la anga lililo katikati ya dunia lilivyoiondoa Dunia tambarare ya kijiografia, ndivyo pia imani ya kwenye Biblia ilivyohamishwa na imani ya kwenye nadharia dhahania za wanadamu. Bila shaka, hilo lilifanywa na mdanganyifu mkuu, kwa kuwa imani kwenye kielelezo cha uumbaji ilidhoofishwa, ndivyo imani kwenye Maandiko mengine yote ikadhoofishwa pia. Kutoamini uwepo wa Mungu kulienea zaidi na walimu wa uongo wakazidi kuwa walegevu, wakisawazisha hali ya pigo dhidi ya Neno la Mungu. Kifaa hiki cha Shetani (dhana ya dunia kulizunguka jua) kilikuwa na ufanisi sana kwenye kuwa ni hatua ya kwanza kuelekea kwenye mageuzi na kumkana Mungu, kiasi kwamba yeyote anayethubutu kuhoji jambo hilo, hata miongoni mwa

Wakristo, anasemekana kuwa ni mpumbavu.

## Dunia Inayozunguka na Mlipuko Mkubwa

Sio tu kuwa mtindo wa dhana ya dunia kulizunguka jua uliileta nadharia ya Darwin ya mageuzi, lakini pia ulisababisha nadharia ya Big Bang. Nadharia ya Big Bang ni sehemu isiyoweza kutenganishwa ya sayansi inayohitajika ili kuendeleza dhana ya dunia kulizunguka jua. Bila nadharia ya Big Bang, hakuna maelezo ya kisayansi ya mwendo wa sayari. Kwenye makala iliyochapishwa na *The New York Times*, Robert Jastrow, mkurugenzi wa zamani wa Taasisi ya NASA ya Goddard ya Mafunzo ya Anga, anasema:

> Picha ya jumla ya kisayansi inayoongoza kwenye nadharia ya big bang inajulikana sana. Tumekuwa tukifahamu kwa miaka 50 kuwa tunaishi kwenye ulimwengu unaopanuka ambamo galaksi zote zinazotuzunguka zinasogea kando na nyingine kwa kasi kubwa sana. Ulimwengu unavuma mbele ya macho yetu, kana kwamba tunashuhudia matokeo ya mlipuko mkubwa. Tukirudisha nyuma mwendo wa galaksi zinazosogea nje kwa wakati, tunaona kuwa zote zinakusanyika pamoja, kama tunavyoweza kusema.[46]

Kulingana na mwanasayansi huyu wa kisasa, Big Bang ndio chanzo cha mwendo wote wa sayari. Ndio sababu ya Dunia kujichaji kupitia angani kwa kasi hiyo kubwa. Mkristo ambaye haamini kwenye Big Bang, lakini bado anaamini kuwa Dunia inazunguka kwenye mhimili wake, inazunguka jua, na kusafiri kupitia anga, huyo anakuwa anakabiliwa na shida. Kwa kuwa wanashutumu maelezo yanayotolewa na sayansi ya kisasa kuhusu mwendo wa Dunia, ni lazima watoe maelezo yao wao wenyewe kuhusu mzunguko wa Dunia kuzunguka jua (kilometa 107,000 kwa saa) na kujichaji kwa Dunia kupitia anga (kilometa 828,000 kwa saa). Hata hivyo, hakuna maelezo ya mwendokasi huo wa kustaajabisha yanayoweza kupatikana kwenye Biblia. Kinyume chake, Biblia inasema mara kwa mara kuwa Dunia ni imara na haiwezi kuhamishwa, na zaidi, kuwa jua ambalo linatembea kwenye mzunguko juu ya Dunia! Kwa hiyo, kwa kuwa hakuna maelezo ya kasi hizi yanayoweza kupatikana kutoka kwenye Maandiko, mtu hawezi kuishika sayansi ya kisasa kwenye kuamini kuwa Dunia inazunguka kwa kasi ya jua, na bado kukataa maelezo ya kisayan-

si ni kwanini inafanya hivyo. Ni lazima Mkristo akubali kwamba sayari zilianzishwa na nishati ya Big Bang (na hivyo kukubali mageuzi ya imani ya kupinga uwepo wa Mungu), au kuukemea kabisa mtindo wa dunia kulizunguka jua na kuthibitisha kuwa Dunia imesimama kama Biblia inavyosema.

Ni njia iliyo wazi iliyoje ambayo muamini angeipata kwa manufaa yake kama tu angechukua yale ya Biblia! Hakuna uvumi kuhusu asili ya kasi hizi zinazodhaniwa kuwa ni za lazima, kwani kutosogea kwa Dunia kunathibitishwa mara kwa mara kwenye Maandiko Matakatifu. Mtu anayeamini kuwa Dunia ni tambarare, tofauti na yule anayedai kuwa dunia inazunguka jua angani, anatoa uthibitisho baada ya uthibitisho wa kielelezo chake kutoka kwenye Maandiko, na si uvumi wa sayansi ambao ni wa uongo.

Kwa hakika, uadilifu wa Mkristo anayeamini kuwa Dunia ni tambarare umetiwa doa hasa na mkabala wake halisi, wa ukweli wa simulizi ya uumbaji ya Mwanzo. Ni njia hii ambayo inamfanya akubali kuwa uumbaji ulichukua siku sita halisi ili kukamilishwa. Hapa imani ya kweli kwenye Mungu inadhihirishwa. Hata hivyo, mtu asiishie kwenye hitimisho la Mwanzo 1, kwa kuwa uaminifu na maadili ya mtu kiukweli yanatiwa majaribuni na yale ambayo Mungu aliyasema baada ya siku hizo sita za mwanzo. Kwenye Mwanzo sura ya 2, tunasoma hivi:

> Mwanzo 2:1 Basi mbingu na nchi zikamalizika, na jeshi lake lote.
> 2:2 Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya; akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya.
> 2:3 Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Mungu alistarehe, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoiumba na kuifanya.

Mungu alipumzika mwishoni mwa kazi Yake. Akaibariki siku ya saba na kuitakasa. Kwenye hilo tendo, Mungu aliagiza kuwa viumbe Vyake vyenye akili navyo vingeacha kufanya kazi zao siku ya saba ya kila juma, ili wapate kukumbuka jinsi ambavyo "kwa siku sita BWANA alifanya mbingu na nchi, akastarehe kwa siku ya saba na kupumzika." Kutoka 31:17. Ili kusisitiza umuhimu wa ukumbusho huu, Sabato ilifanywa kuwa ni sehemu

ya amri kumi alizopewa Musa kwenye Mlima Sinai. Hata hivyo, Sabato ina asili yake si kwa Waebrania au Wayahudi, lakini kwa Adamu na Hawa, ambao waliitunza Sabato na Mungu kwenye bustani ya Edeni. Huu ndio ukumbusho ambao Daudi anarejelea anaposema: "Amefanya ukumbusho wa matendo yake ya ajabu;" Zaburi 111:4.

Ni hakika, Sabato ya siku ya saba ililetwa kwa mwanadamu ili kumkumbusha kazi za ajabu za Mungu za uumbaji. Hii ndiyo sababu kwenye Kutoka 31:17, Mungu anaielezea Sabato kuwa ni ishara ya utii kati yake na watu wake. Kwenye kuishika Sabato, wanadamu huyakiri mamlaka ya Mungu kama Muumba, na hivyo kujitofautisha wenyewe kama watu wake. Kwa hiyo Sabato imetumika kama sehemu ya kuugawanya wakati wote. Kwa maana kwenye nyakati ambapo imani ya miungu mingi ilitawala, na asili ya maisha ilihesabiwa kwa miungu mingi ya kipagani, au kwenye enzi ya kumkana Mungu kama vile leo, wakati nadharia ya mageuzi inapoenea, utunzaji wa Sabato—kama ufahamu wa Mungu wa Biblia kama Muumba—inabakia kuwa ndio ishara muhimu ya utiifu Kwake.

Kwa hivyo, muamini wa kuwa Dunia ni tambarare ambaye huifuata siku ya Jumapili, lakini akawa anaamini kwenye siku sita halisi za uumbaji, anakabiliwa na tatizo kubwa. Kimsingi, imani yake kwenye simulizi ya kweli ya uumbaji haifanyiki tena kama anakataa kushikilia ukumbusho ambao Mungu aliutoa kwa heshima ya simulizi hiyo. Muda wote huo, mtu anayeamini kuwa Dunia ni tambarare ameacha sayansi ya uongo ya wanadamu ili kuishikilia sayansi ya ukweli ya Neno la Mungu. Lakini akiamua kuifuata Jumapili (siku ya kwanza ya juma), anafanya mambo ambayo ni kinyume kabisa. Fikiria majigambo yafuatayo yaliyotolewa na Kanisa Katoliki la Roma kuhusu uhamisho wa Sabato kuipeleka Jumapili.

> Bila shaka Kanisa Katoliki linadai kuwa mabadiliko hayo yalikuwa ni matendo yake…Na matendo hayo ni ALAMA ya uwezo wake wa kikanisa na mamlaka kwenye masuala ya kidini.[47]
>
> Kanisa [Katoliki] lipo juu ya Biblia, na uhamisho huu wa ufuatiliaji wa Sabato ni uthibitisho wa huo ukweli.[48]
>
> Lakini kwa kuwa Jumamosi, wala si Jumapili, imetajwa kwenye Biblia,

je, haishangazi kuwa watu wasio Wakatoliki, wanaodai kuichukua dini yao moja kwa moja kutoka kwenye Biblia na si kutoka kwenye Kanisa, wanaiadhimisha Jumapili badala ya Jumamosi? Ndiyo, bila shaka, haiendani; lakini badiliko hili lilifanywa yapata karne kumi na tano kabla ya Uprotestanti kuzaliwa, na kufikia wakati huo desturi hiyo ilizingatiwa ulimwenguni pote. Wameendeleza desturi hiyo ingawa inategemea mamlaka ya Kanisa Katoliki na si juu ya maandishi yoyote yaliyo wazi kwenye Biblia. Maadhimisho hayo yanasalia kuwa ni ukumbusho wa Kanisa Mama ambalo madhehebu yasiyo ya Kikatoliki yalijitenga nalo—kama vile mvulana anayekimbia nyumbani lakini bado akiwa ameibeba picha ya mama yake au kiremba cha nywele zake.[49]

Hatimaye, kwa kuiadhimisha Jumapili, muamini wa Dunia tambarare anaisaliti sheria yake mwenyewe kuhusu tafsiri halisi ya Maandiko kwa kuyapendelea maoni ya wanadamu. Kwa kweli, kwa kuchagua kuiweka siku ya kwanza mahali pa siku ya saba, muamini wa Dunia kuwa ni tambarare anapuuza ukumbusho ule ule uliowekwa ili kuheshimu simulizi ya Mwanzo ya uumbaji ambayo yeye huistahi sana!

Kwa njia tofauti, bado kuna tabaka lingine ambalo linausaliti mtazamo wao wa kifasihi unaodhaniwa kwenye Mwanzo. Mkristo anaweza kuishika vema Sabato ya siku ya saba kama ukumbusho wa siku sita halisi za uumbaji. Lakini kama anakataa kile ambacho Maandiko yanakisema kuwa kilifanywa wakati wa siku hizo sita, na kuchagua kukubali kielelezo chenye upinzani kinachokuzwa na sayansi, anaanguka kwenye kosa kama hilo. Kama muangalizi wa siku ya Jumapili, anakataa mamlaka ya Mungu kwa kupendelea mamlaka ya wanadamu. Anaikumbuka Sabato lakini anakisahau kile ambacho kiliamriwa kuadhimishwa na Sabato. Kwenye Zaburi 111, Daudi anatukumbusha ni nini inahusu kushika Sabato kiukweli:

> Zaburi 111:2 Matendo ya BWANA ni makuu, yafikiriwa sana na wapendezwao nayo.
> 111:3 Kazi yake ni heshima na adhama, Na haki yake yakaa milele.
> 111:4 Amefanya ukumbusho wa matendo yake ya ajabu; BWANA ni mwenye fadhili na rehema.

Matendo ya ajabu ya Mungu yalifanywa ili yakumbukwe. Na kazi hizi

zimeainishwa waziwazi kwenye sura ya kwanza ya Biblia, ambapo hakuna pendekezo hata kidogo la tufe inayozunguka jua. Kinyume chake, tumeona kuwa jua liliumbwa siku ya nne, lilipowekwa ndani ya anga lililoundwa na anga la juu ya Dunia. Kwa hivyo, muumini wa ulimwengu ambaye anashikilia dhana ya asili ya ulimwengu mbele ya vifungu visivyohesabika vya Maandiko hawezi kuhesabiwa kuwa ameyatafuta matendo makuu ya Bwana na kuyafurahia, kwa kuwa ameyakataa.

Walakini, kwa shida za matabaka yote mawili, kuna suluhisho rahisi: lililokubali Neno la Mungu kwa ukamilifu. Kisha, uvumi na falsafa ya wanadamu haitahitajika tena ili kudumisha nafasi isiyofaa ya mtu, na kila moja itakuwa na mamlaka ya kuitegemea kauli ya 'Bwana Asema'.

Ila ole, badala ya kuukubali ufunuo wenye mamlaka isiyopingika ya Maandiko, wengi huibuka dhidi ya ujumbe huo kwa sababu haufai kwao, wakikusanya dhihaka na dharau kwa wanaouunga mkono. Hata hivyo, aina hii ya dharau haipaswi kushangaza, kwa kuwa Petro alitabiri juu ya hawa wenye dhihaka tangu zamani sana.

Akiwalinganisha wale waliopita kabla ya gharika waliolikataa Neno la Mungu na kumdhihaki mjumbe Wake, na wale wanaofanya vivyo hivyo kwenye siku za mwisho, Petro anaonya kwa kusema hivi: "Siku za mwisho watakuja na dhihaka zao watu wenye kudhihaki, wafuatao tamaa zao wenyewe". Badala ya kutegemea Maandiko kama muongozo wao wa mambo yote, hawa wanaodhihaki huchagua kufuata mielekeo yao wao wenyewe. Kuwa Petro anamrejelea Mkristo na si walimwengu inaoneshwa na maneno yao ya dhihaka: "na kusema, *Iko wapi ahadi ile ya kuja kwake?* Kwa maana, tangu hapo baba zetu walipolala, vitu vyote vinakaa hali hiyo hiyo, *tangu mwanzo wa kuumbwa*." 2 Petro 3:3-4. Kama vile watu wasiomcha Mungu walivyomdhihaki Noa alipohubiri ujumbe wa mwisho wa rehema wa Mungu kwenye ulimwengu wa kale, vivyo hivyo ujumbe wa mwisho wa rehema wa Mungu utadhihakiwa na jamii hii ya wale wanaojiita waamini. Lakini wao ni akina nani?

Mambo mawili yanaweza kuthibitishwa kuhusu hawa wanaodhihaki mambo ya Mungu nyakati za mwisho. Kwanza, ni waumini wa ujio wa pili wa Bwana Yesu Kristo. Na pili, wao ni wabunifu.

Zaidi ya hayo, kwenye aya inayofuatia, upungufu mmoja unaotofautishwa kwenye imani yao unatambuliwa. Petro anaonesha fundisho moja la kanuni ambalo wanalikataa, akisema: “Maana hufumba macho yao wasione neno hili ya kuwa zilikuwako mbingu tangu zamani, na nchi pia, *imefanyizwa* kutoka katika maji, na ndani ya maji, kwa neno la Mungu;” 2 Petro 3:5.

Ni suala la uumbaji ambalo hawa wanaodhihaki hulishughulikia. Walakini, hapo awali Petro alithibitisha kuwa kundi hili linaamini kwenye uumbaji, kwa kuwa walisema: "Vitu vyote hubakia kama vile vilikuwepo tangu mwanzo wa *kuumbwa*". Tafadhali tambua jambo hili linaloonekana kupingana. Sasa kwa nini Petro anasema kuwa ni kwa makusudi kwamba watu hawa hawajui kwa hiyari juu ya vipengele fulani vya uumbaji? Je, watu wanaoamini uumbaji hawaamini kuwa Mungu alizungumza ili vitu vyote viwepo? Kwa kuibua kitendawili hiki tunafika kwenye ugunduzi wa kushtua.

Ingawa ndugu hawa wanakiri kuwa uumbaji ni asili ya uhai, Petro anaelezea mambo mawili hususan ya *simulizi* ya uumbaji wa Mwanzo ambayo hawa wanaodhihaki enzi hizi za siku za mwisho hawalijui *kwa makusudi*. Lizingatie neno kwa makusudi. Baada ya kuwasilishwa kwa ushahidi, tabaka hili limechagua kupuuza yale ambayo Mungu amewafunulia kuhusu uumbaji wake. Ujinga wao ni wa makusudi.

Petro anaendelea kuwakemea kwa kueleza kwa undani kipengele cha kwanza cha suala la Mwanzo ambalo hawa wenye dhihaka wanalipuuza kimakusudi: “kuwa mbingu zimekuwa ni za kale kwa *neno* la Mungu”. Hapa, Petro anaelekeza kwenye kitu ambacho kilifanywa, kwa kuwa asili yake ilikuwa ni “kwa neno la Mungu”; rejeleo la wazi la kazi ya Mungu ya uumbaji Alipozungumza na ikafanyika kama Alivyotaka.

Kama ambavyo imethibitishwa, anga ni sehemu ya muhimu ya "mbingu" kulingana na Maandiko, na ilikuwa ni angani ambapo Mungu aliweka nguvu ya Neno Lake. Kwa uhakika, angani ambamo ndege huruka na nyota hupita zipo tu kwa sababu ya muundo ambao ni thabiti. Kwa maana ni anga ambalo liligawanya wingi wa maji ndani ya maji ya "chini ya anga" na yale "yaliyokuwa juu ya anga". Kwa hiyo, ni sifa hii kuu ya mbingu—

anga—ambayo wanaodhihaki nyakati hizi za mwisho wanaikataa. Wamechagua kupuuza muundo ambao Mungu aliutandaza juu ya Dunia, kwa kuwa haupatani na dhana zao za kisayansi. Hivyo, inaweza kusemwa kiukweli kuwa kwa hiari yao hawajui mbingu zilizokuwepo tangu zamani.

Bado huu sio ukweli pekee ambao kundi hili la waumini huupuuza. Pia, wanakataa ukweli wa Biblia kuwa "na nchi pia, imefanyizwa kutoka katika maji, na ndani ya maji," 2 Petro 3:5. Hili ni dokezo lingine la wazi la Mwanzo na Maandiko mengine ambayo yanaonesha Dunia ikiwa imekaa juu ya maji ya kilindi kikubwa, ikisimama kimuujiza juu ya nguzo zake kwenye msingi wa maji. Muumini wa kielelezo cha dhana ya dunia kulizunguka jua na dunia yake inayozunguka angani hawezi kuvikubali hivi vifungu, kwa kuwa vinatofautiana sana na kielelezo chao pendwa cha kisayansi. Badala yake, kama inavyoshuhudiwa hii leo, wao huinuka dhidi ya ujumbe huu, wakiwadhihaki na kuwacheka wale walio na ujasiri wa kuwa na msimamo wao juu ya yale ambayo Biblia inafundisha waziwazi.

Kwa dharau inayooneshwa hadi sasa na wale wanaojiita Wakristo ili kutoa uthibitisho wa wazi wa Biblia, si vigumu kufikiria jinsi ambavyo ndugu hao hao, wakiendelea na mwendo wao, watakavyoishia kuwa ndio wale wale waliotabiriwa na Petro, ambao wataudhihaki ujumbe wa rehema unaokuja hivi karibuni kwenye huu ulimwengu wa sasa. Kwa hakika, ujumbe wa mwisho utatolewa na wale ambao kwa kweli wanaishi kwa kila neno litokalo kwenye kinywa cha Mungu, na si kwa wale wanaochagua na kuchagua kile kinachowafaa.

Hatimaye, endapo mtu anaamini kuwa Mungu aliiumba dunia ambayo inazunguka zunguka angani, basi ni lazima simulizi ya Mwanzo kwa ujumla ikataliwe. Walakini, endapo mtu atachukua mkabala ambao ni halisi, usio na makosa kwenye Mwanzo 1, basi kukubali kielelezo cha Ardhi ni tambarare ndiyo hitimisho pekee lenye mantiki. Hili linasisitizwa na David H Bailey, mtaalamu wa dhana ya dunia kulizunguka jua, kwenye makala yake ya *What was the Ancient Biblical Cosmology?* anasema:

> Bila shaka, leo hii karibia wasomaji wote wanaiona mistari hizi kama nyenzo za kifasihi zinazosisitiza utukufu wa Mungu, si kama ukweli halisi wa kisayansi...Huu, kwa ufupi, ndiyo ugumu mkuu katika kuuchukua

> *mtazamo halisi, usio na makosa kwenye Biblia* na kuutumia mtazamo huu wa ulimwengu kama msingi wa mtazamo wa uumbaji wa dunia ambayo ni changa: sio tu kwamba mtazamo kama huo unapingana kabisa na kiasi kikubwa cha taarifa za kisayansi, lakini pia *ingehitaji mtu wa karne ya 21 kuchukua dhana ya kale ya asili ya ulimwengu na kuwa mtetezi wa kwamba dunia ni tambarare!*[50]

Hii inaturudisha pale tulipoanzia. Ili kuepusha jina la dharau la 'dunia tambarare', Wakristo wanachagua kutafsiri vifungu vingi vya Biblia kwa msingi wa mashairi, na kuacha mtazamo halisi wa Mwanzo. Lakini kama vile mwanaastronomia Mjesuiti Guy Consolmagno anavyosema, kudumisha mtazamo halisi wa Mwanzo ina maana kuwa ni lazima uamini kwenye Dunia tambarare iliyofunikwa na kuba! Kwa kweli, kwenye mahojiano na *FORA TV*, Consolmagno anakumbuka kipindi ambapo alifikiwa na Mkristo aliyedai kuamini simulizi halisi ya Mwanzo. Jibu lake ni la kupendeza sana:

> Mmoja wa vijana hao alinijia na kusema hivi: "Unajua, ninataka tu kukufahamisha, ninaamini kwenye ukweli kamili kuwa uumbaji ulifanywa kwa siku sita kama vile ilivyoelezwa kwenye Kitabu cha Mwanzo. Na hiyo ndiyo dini yangu; Nataka tu ujue hilo mapema." Na ninafikiria, unajua, *kweli umeisoma Mwanzo? Ambapo inasema ulimwengu ni tambarare, na umefunikwa na kuba, na kuna maji juu na chini ya kuba.*[51]

Kwa uhuru, mwanaastronomia huyu Mjesuiti anakubali kile ambacho ni kinaonesha uhalisi wa jinsi Mwanzo inavyohusishwa. Hata hivyo, badala yake akachagua kuunga mkono msimamo wa sayansi, yeye anasema hivi:

> Ni picha ya aina gani ya Mungu ninayopata mwisho wa siku ninapoona kuwa *ulimwengu sio tu kuba juu ya Dunia tambarare, kama jinsi kitabu cha Mwanzo kinavyofafanua*, lakini ikawa ni idadi isiyo na kikomo ya aina mbalimbali za maada?—sayansi inafanya nini kuyapanua maoni yangu kuhusu jinsi ambavyo Mungu ni mkuu. Na kama nilivyosema hapo awali, *imani yangu ya kimsingi ya jinsi ambavyo ulimwengu unafanya kazi, ambayo haiwezi kuthibitishwa na sayansi, ni mawazo ninayoanza nayo* kabla sijaunda mfumo wa kimantiki.[52]

Mwanasaikolojia mwingine maarufu, Neil deGrasse Tyson, alitoa mfano

unaofanana alipoulizwa kama imani na sababu zinaweza kusuluhishwa. Kwenye kulijibu hili swali, Tyson alisema:

> Sidhani kuwa zinaweza kupatanishwa....Kwa mfano, kama haujui lolote kuhusu sayansi, na ukasoma Biblia (Agano la Kale) ambayo kwenye Kitabu cha Mwanzo inasimulia. asili, na nikakuambia, nipe maelezo yako ya ulimwengu wa asili kulingana na hii tu. Unaweza kusema ulimwengu uliumbwa kwa siku sita na kuwa nyota ni nuru ndogo tu, ndogo sana kuliko jua, na kwa kweli zinaweza kuanguka kutoka angani kwa sababu ndivyo inavyotokea wakati wa Ufunuo....*Kwa hiyo kuandika tu hayo mambo ina maana haujui mambo hayo ni nini. Hauna hata wazo la namna ambavyo ulimwengu halisi ulivyo. Kwa hiyo kila mtu ambaye alijaribu kutoa matangazo kuhusu ulimwengu unaoonekana kulingana na vifungu vya Biblia alipata jibu lisilo sahihi.* Wakati sayansi inapogundua mambo, na unataka kubakia kwenye kidini, au unataka kuendelea kuamini kuwa Biblia haina makosa, unachoweza kufanya ni kusema, vema, hebu nirudi kwenye Biblia na kuifasiri upya. Kisha ungesema vitu kama, oh hawakumaanisha hivyo kiuhalisi, walimaanisha hivyo kwa njia ya mfano. *Kwa hivyo ufafanuzi huu mzima wa jinsi vifungu vya mashairi vya Biblia ni vya kitamathali na ulikuja baada ya sayansi kuonesha kuwa sivyo mambo yaliyotokea.* Na kwa hiyo watu wa dini walioelimika wanaridhika kabisa na hilo. *Ni wafuasi ambao wanataka kusema kuwa Biblia ni ukweli halisi wa Mungu* na wanataka kuiona Biblia kama kitabu cha maandishi ya sayansi ambapo wanabisha hodi kwenye milango ya sayansi ya shuleni...[53]

Kwenye haya mahojiano na *Moyers and Company*, Tyson anaeleza jinsi imani za “wanaoamini kwenye msingi fulani wanapotaka kusema kuwa Biblia ni ukweli halisi wa Mungu” zinavyopingana kabisa na uvumbuzi wa kisayansi. Anaendelea kusema kuwa "kila mtu ambaye alijaribu kutoa matangazo kuhusu ulimwengu unaoonekana kulingana na vifungu vya Biblia alipata jibu lisilo sahihi". Na zaidi ya hayo, kuwa ilikuwa tu “baada ya sayansi kuonesha kuwa hivi sivyo mambo yalivyotokea”—rejelea simulizi ya uumbaji ya Mwanzo—ndipo Wakristo wengi walilazimika kutafsiri upya vifungu vya Biblia kwa maana za kitamathali, ili kuwa na maelewano na sayansi.

Enyi marafiki, tusiwe miongoni mwa wale wenye dhihaka wanaokana uk-

weli maalum wa uumbaji kwa kuipendelea "elimu iitwayo elimu kwa uongo". Na tuwe miongoni mwa wale wanaoegemeza ufahamu wao kwenye Biblia, badala ya mawazo yasiyoweza kuthibitishwa ya wanadamu. Hakika, Mungu huziona nyakati za ujinga wetu, lakini mara nguvu ya ukweli inapofunua mawazo yetu yaliyo potofu, tunawajibika kwa kukataliwa kwake.

Kitabu cha Matendo kinatuambia kuwa Yesu hawezi kurudi "hata zije zamani za kufanywa upya vitu vyote, zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu." Matendo 3:21. Tumeona wazi kuwa Biblia inafundisha juu ya Dunia ambayo ni tambarare, isiyozunguka. Ni lazima ukweli huu urejeshwe na watu wa Mungu kabla ya Bwana kurudi. Kwa maana mabaki ya Mungu yamefafanuliwa kuwa ni yenye ubikira na hayana unajisi, kumaanisha kuwa yapo huru kutokana na mafundisho yote ya uongo.

Ingawa bila shaka kuukubali ukweli huu usiopendwa na watu wengi kutakuwa na dhihaka na dharau, hata hivyo hatupaswi kuogopa. Hatimaye, hili ni suala ambalo kila Mkristo atalazimika kukabiliana nalo, kama ilivyokuwa kwa wanamatengenezo wa zamani. Swali la kila mtu binafsi kujipima litakuwa ni: Je, nitasimama juu ya mafundisho yasiyokosea ya neno la Mungu pamoja na manabii wa Biblia na warekebishaji wa Kiprotestanti? Au nitasimama juu ya madai ya sayansi ya kisasa, ambayo inakiri waziwazi kuwa imeharibu kielelezo cha uumbaji kilichotolewa na Mungu?

Enyi kaka na dada, kama mmesadikishwa kuwa kile ambacho kimeletwa kwenu ni cha kweli, basi mkatende kulingana na usadikisho wenu, "ili imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu." 1 Wakorintho 2:5.

# FAHARASA:
# DHANA ZA DUNIA KUWA NI DUARA ZILIZOPO KWENYE BIBLIA

## Uso wa Dunia

Kwenye jiometri, uso hufafanuliwa kama upande wa kitu. Ni uso tambarare. Kwa mfano, mchemraba una nyuso sita. Tufe ndio umbo pekee ambalo halina nyuso zozote.

Mwanzo 1:29, 6:1, 7:3-4, 8:9, 41:56.
Kutoka 32:12, 33:16.
Hesabu 12:3.
Kumbukumbu la Torati 7:6.
1 Samweli 2:10, 20:15.
1 Wafalme 13:34.
Ayubu 37:12, 38:13-14.
Yeremia 25:26.
Ezekieli 34:6, 38:20, 39:14.
Amosi 9:6.
Luka 21:35.
Ufunuo 1:7.

## Mduara; Sio Tufe

Linganisha Isaya 40:22 na Isaya 22:18. Isaya alijua jinsi ya kuuelezea mpira au tufe, lakini badala yake alichagua kuielezea Dunia kama duara (ambalo ni tambarare).

## Mwisho wa Dunia

Tufe halina nyuso, kingo, au ncha. Kwa kulinganisha, diski tambarare ina uso kwa kuongezea kingo na mwisho wake.

Kumbukumbu la Torati 28:64, 33:17.
Ayubu 37:3, 38:13.
Zaburi 46:9, 48:10, 59:13, 72:8, 98:3.
Mithali 8:29, 17:24, 30:4.

Isaya 41:9, 45:22, 48:20, 49:6, 52:10.
Yeremia 16:19, 25:31.
Danieli 4:10-11,20.
Mika 5:4.
Zekaria 9:10.
Matendo 13:47, 17:26.

## Mungu Anayazuia Maji

Mungu aliyaamuru maji yasiasi amri yake. Anayazuia yasianguke kutoka kwenye ncha za Dunia.

Ayubu 26:10, 38:11.
Zaburi 104:9.
Mithali 8:27-29.

## Dunia Imejengwa Juu ya Misingi

Dunia imejengwa juu ya misingi na nguzo.

1 Samweli 2:8.
Ayubu 9:6.
Ayubu 38:4-6.
Zaburi 75:3, 102:25, 104:5.
Isaya 48:13, 51:13.
Yeremia 31:37.
Zekaria 12:1.

## Jua Husogea

Jua hutembea huku Dunia ikiwa imetulia. Mungu aliagiza kuwa itakuwa ni kazi ya jua na mwezi kuzalisha siku, usiku, majira na miaka.

Mwanzo 1:14-19.
Yoshua 10:12-14.
2 Wafalme 20:8-11.
1 Mambo ya Nyakati 16:30.
Zaburi 19:1-6, 96:10.
Amosi 8:9.
Zekaria 1:11.

## Anga Hututenganisha na Maji ya Juu

Anga hilo linafafanuliwa kuwa ni hema au kuba ambamo ndege na vile vile jua, mwezi, na nyota hukaa. Anga liliundwa ili "likayatenge maji na maji". Maji yaliyo juu ya anga yapo hadi leo, na yametenganishwa na yale yaliyo chini ya anga, kama vile bahari na vilindi vikuu.

Mwanzo 1:1-2, 6-8, 7:11, 8:2.
Ayubu 37:18.
Zaburi 148:4.
Isaya 40:22.

## Mungu Yu Karibu Zaidi Kuliko Unavyofikiri

Dunia inaelezewa kuwa ni kiti cha miguu cha Mungu.

Kutoka 24:10.
Kumbukumbu la Torati 33:26.
Zaburi 68:4, 33-34, 104:1-3.
Maombolezo 2:1.
Ezekieli 1:26.
Mathayo 5:34,35.
Matendo 7:49.




*Ramani Mpya ya Ulimwengu Sanifu (1892)*
*na Alexander Gleason*
*Msabato na Mhandisi*

# MAELEZO YA MWISHO

1 John Jefferson Davis, "When Does Personhood Begin?," Eternity N Vol 30, October 1979, p41.
2 G. L. Robinson, Leaders of Israel (New York: Association Press, 1913), 2. https://ncse.com/image/ancient-hebrew-cosmology
3 Daniel Esparza, "When the Earth was flat: a map of the universe, according to the Old Testament," Aletia. Jul 07, 2016. https://aleteia.org/2016/07/07/when-the-earth-was-flat-a-map-of-the-universe-according-to-the-old-testament/
4 Kaufmann Kohler, Emil G. Hirsch, "Cosmogony: Earlier Versions," Jewish Encyclopedia. http://www.jewishencyclopedia.com/articles/4684-cosmogny#2736%3E
5 "H7549," The Strong's Concordance, e-Sword Bible App.
6 Albert Barnes, "Job 37:18," Albert Barnes Notes on the Whole Bible. https://biblehub.com/commentaries/barnes/job/37.htm
7 "H3835," The Strong's Concordance, e-Sword Bible App.
8 "White Sapphires," The Natural Sapphire Company. https://www.thenaturalsapphirecompany.com/white-sapphires/
9 "Sapphires: Types, Colors, Descriptions, Origins and Details," The Natural Sapphire Company. https://www.thenaturalsapphirecompany.com/t-education_sapphires/
10 Bill Flavell, "Five days that unravel the Bible," Atheist Alliance International, April 5, 2018. https://www.atheistalliance.org/thinking-out-loud/five-days-that-unravel-the-bible/
11 Kaufmann Kohler, Emil G. Hirsch, "Cosmogony: Earlier Versions," Jewish Encyclopedia. http://www.jewishencyclopedia.com/articles/4684-cosmogony#2736%3E
12 "Geoid," Encyclopaedia Britannica. https://www.britannica.com/science/geoid
13 "Aristarchus of Samos," Britannica Kids. https://kids.britannica.com/students/article/Aristarchus-of-Samos/599426
14 Andrew Dickson White, A History of the Warfare of Science with Theology in Christendom, Vol. I" (New York: D. Appleton & Company, 1897),
15 Robert J. Spitzer, "A Catholic Response to Neil deGrasse Tyson's

Cosmos—Filling in the Intellectual Gaps," Magis Centre. https://magis-center.com/a-catholic-response-to-neil-degrasse-tysons-cosmos-filling-in-the-intellectual-gaps/

16 Benjamin G. Wilkinson, Our Authorized Bible Vindicated (Washington: 1930), Chapter 4. http://www.sdadefend.com/Living-Word/Wilkinson/authorizedbible4.htm

17 Martin Luther, Tabletalk (1539).

18 "Thomas, Cardinal Wolsey," Encyclopedia Britannica. https://www.britannica.com/biography/Thomas-Cardinal-Wolsey

19 Cardinal Wolsey quoted in The Life and Raigne of King Henry the Eighth by Edward Lord Herbert of Cherbury (London: Printed by E.G. for Thomas Whitaker, 1649), 157-158.

20 F. Tupper Saussy, Rulers of Evil (New York: HarperCollins, 2001), 23-24.

21 J. H. Merle D'aubigne, History of the Reformation of the Sixteenth Century, Volume 1, translated by Henry Beveridge (Glasgow: William Collins, 1845), 74.

22 Copernicus, De revolutionibus, I.10, CGA, II, pp. 20.12-21.1.

23 Hermes Trismegistus, Hermetica: The Greek Corpus Hermeticum and the Latin Asclepius in a New English Translation, translated by Brian P. Copenhaver (Cambridge: Cambridge University Press, 1995): 59,61.

24 J. H. Merle D'aubigne, History of the Reformation of the Sixteenth Century, Volume 2, translated by Henry White (New York: American Tract Society, 1848), 109.

25 John Calvin, "Sermon on 1 Corinthians 10:19-24", Calvini Opera Selecta, Corpus Refomatorum, Vol 49, 677. Trans. by Robert White in "Calvin and Copernicus: the Problem Reconsidered", Calvin Theological Journal 15 (1980), p 233-243, at 236-237

26 John Calvin, "Ps 93:1," Commentary on the Psalms: Volume IV.

27 John Calvin, The Institutes of the Christian Religion, trans. Henry Beveridge (Edinburgh: Calvin Translation Society, 1846), Book 1, 5:11. https://oll.libertyfund.org/titles/535>

28 Andrew Dickson White, A History of the Warfare of Science with Theology in Christendom (New York: D. Appleton & Company, 1896), 126-128.

29 "Counter-Reformation," Encyclopaedia Britannica. https://www.

britannica.com/event/Counter-Reformation
30 Nicolaus Copernicus, "Dedication of the Revolutions of the Heavenly Bodies to Pope Paul III (1543)", The Harvard Classics Volume 39: Prefaces and Prologues to Famous Books (New York : P.F. Collier & Son, c1909-10), 52.
31 Robert J. Spitzer, "A Catholic Response to Neil deGrasse Tyson's Cosmos – Filling in the Intellectual Gaps," Magis Center. https://www.magiscenter.com/a-catholic-response-to-neil-degrasse-tysons-cosmos-filling-in-the-intellectual-gaps/
32 Guy Consolmagno, "Interview with Brother Guy Consolmagno", Astrobiology Magazine, May 12, 2004. https://www.astrobio.net/cosmic-evolution/interview-with-brother-guy-consolmagno/
33 Johannes Kepler, Book V: Of the Harmony of the World, trans. E. J. Aiton, Alistair Matheson Duncan, Judith Veronica Field (American Philosophical Society, 1997), 391.
34 "Johannes Kepler," New World Encyclopedia. https://www.newworldencyclopedia.org/entry/Johannes_Kepler
35 "The Law of Universal Gravitation," PhysicsLAB. http://dev.physicslab.org/Document.aspx?doctype=3&filename=UniversalGravitation_UniversalGravitation.xml
36 "Graviton," Encyclopaedia Britannica. https://www.britannica.com/science/graviton
37 Michael Greshko, "Isaac Newton's Lost Alchemy Recipe Rediscovered," National Geographic, April 4, 2016. https://news.national-geographic.com/2016/04/160404-isaac-newton-alchemy-mercury-recipe-chemistry-science/
38 Isaac Newton, quoted by William Scott Shelley, Science, Alchemy and the Great Plague of London (New York: Algora Publishing, 2017), 91.
39 Tessa Morrison, Isaac Newton's Temple of Solomon and his Reconstruction of Sacred Architecture (Newcastle Australia: Springer Basel, 2011), 25
40 "Cambridge University puts Isaac Newton papers online," BBC News, 12 December 2011. https://www.bbc.com/news/uk-england-cambridgeshire-16141723
41 M. White, Isaac Newton: The Last Sorcerer (Basic Books: 1997), 2-3.
42 Andrew Dickson White, A History of the Warfare of Science with

Theology in Christendom, Vol. I" (New York: D. Appleton & Company, 1897), 15.
43 Holli Riebeek, "Planetary Motion: The History of an Idea That Launched the Scientific Revolution," Earth Observatory NASA, July 7, 2009. https://www.earthobservatory.nasa.gov/features/OrbitsHistory
44 John H. Lienhard, "No. 1168: Voltaire And Science," The Engines of Our Ingenuity, University of Houston. https://www.uh.edu/engines/epi1168.htm
45 "Signs of earliest stars seen from Australia," Commonwealth Scientific and Industrial Research Organisation. https://www.csiro.au/en/News/News-releases/2018/Signs-of-earliest-stars-seen-from-Australia As reported in the journal Nature volume 555, pages 67–70 (01 March 2018) by Judd D. Bowman, Alan E. E. Rogers, Raul A. Monsalve, Thomas J. Mozdzen & Nivedita Mahesh. https://doi.org/10.1038/nature25792
46 Robert Jastrow, "Have Astronomers," The New York Times, June 25, 1978. https://www.nytimes.com/1978/06/25/archives/have-astronomers-found-god-theologians-are-delighted-that-the.html
47 Letter from C.F. Thomas, Chancellor of Cardinal Gibbons on October 28, 1895.
48 "Sabbath Observance," The Catholic Record, Volume XLV Edition 2342, September 1, 1923, p4. http://biblelight.net/c-record.htm
49 John A. O'Brien, The Faith of Millions: the Credentials of the Catholic Religion Revised Edition (Our Sunday Visitor Publishing: 1974), 400-401.
50 David H Bailey, "What was the Ancient Biblical Cosmology?" Science Meets Religion, January 16, 2018.
51 Guy Consolmagno, "Was the Bible Meant to be Taken Literally?", FORA.tv, published on Youtube on March 27, 2008. https://www.youtube.com/watch?v=wUyiQufyiK0
52 Guy Consolmagno, "Interview with Brother Guy Consolmagno", Astrobiology Magazine, May 12, 2004. https://www.astrobio.net/cosmic-evolution/interview-with-brother-guy-consolmagno/
53 "2014 Neil DeGrasse Tyson Interview on Bill Moyers (Full)", Moyers and Company, Published on Youtube on August 10, 2014. From 38:25. https://www.youtube.com/watch?v=XjTZzP95ugo

Kwa taarifa zaidi tembelea:
www.earthenvessels.org.au





Kufuatia uchunguzi wa kina wa Neno la Mungu na historia ya asili ya ulimwengu, mtu anafikia hitimisho la msingi.

Aidha manabii wa Biblia na warekebishaji walikosea, au kila kitu ambacho umeambiwa kuhusu Dunia ni uongo.





EARTHEN VESSELS
2 CORINTHIANS 4:7